

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Jumapili, 10 Octoba 2010

Rushwa Ndogo Ndogo Inachafua Taaluma ya Utatibu

Rushwa hapa nchini, imejitokeza katika aina mbili; rushwa ndogondogo na rushwa kubwa. Rushwa ndogo ndogo imekuwa tishio kwa Serikali kwani zimeendelea kukithiri katika sekta ya afya. Hali hii siyo tu inawaathiri watu wenye kipato cha chini (wasio na uwezo wa kutoa hongo), bali pia inachafua taaluma ya udaktari nchini.

Hivi karibuni, Sikika imeandika kitabu kutokana na utafiti uliofanyika juu ya rushwa ndogondogo katika huduma za afya, kitabu hicho kinachojulikana kama "[*Rushwa Ndogo Ndogo katika Huduma za Afya Dar es Salaam na Pwani*](#) " kinaonyesha jinsi rushwa inavyojitokeza katika utoaji wa huduma za afya katika wilaya nne za Kinondoni, Temeke, Ilala na Kibaha. Lengo hasa la utafiti huo ni kupima uelewa wa watumia huduma za afya katika rushwa na pia kujua dhima, uzoefu na mchango wao kwa katika kuendeleza vitendo vya rushwa na athari za rushwa kwa wanaotafuta huduma za afya.

Matokeo yanaonyesha kwamba kwa miaka mingi, wanaotoa na kupokea rushwa wanaonekana kuikubali na kuona ni kitendo cha kawaida. Matokeo yake, sehemu kubwa ya jamii inaamini kwamba bila kuhonga hawatahudumiwa ipasavyo. Pale hongo inaporasimishwa katika mifumo ya utoaji wa huduma, hutengeneza matabaka ambapo wenye pesa hupata huduma kukidhi mahitaji yao kuliko tabaka la masikini wasio na uwezo wa kutoa hongo. Hivyo, masikini ndio wanaathirika na matokeo hasi ya rushwa haswa kuongezeka kwa gharama na kupungua kwa ubora wa huduma za afya.

"Rushwa ni tatizo kubwa linalogusa sekta zote, lakini ni tatizo kubwa zaidi katika sekta ya afya kwa sababu inapunguza rasilimali muhimu zilizo tengwa kwa ajili ya kutolea huduma za afya; hupunguza ubora na ufanisi katika huduma za afya na huongeza gharama za kutolea huduma hizo. Vilevile, rushwa inapunguza usawa katika upatikanaji wa huduma za afya kwa kuwakatisha tamaa masikini, ambao wanalazimika kutoa rushwa ili kupata huduma zinazostahili kutolewa bure. Matokeo yake ni kushuka kwa kiwango cha afya na ustawi wa jamii." amesema Irenei Kiria, "Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika

Katika kutathmini uelewa na ushiriki wa watumia huduma za afya katika vitendo vya rushwa, kitabu kimeonesha kuwa mtaalam mmoja kati ya wataalam wa afya watano waliohojiwa (21%) alikiri kupokea hongo. Madaktari waliongoza kwa asilimia kubwa 35% (ambao ni 29 kati ya 85 waliohojiwa), wakifuatiwa na wafanyakazi wa maabara 34% (ambao ni 11 kati ya 32 waliohojiwa). Kundi kubwa la waliohojiwa walikuwa wauguzi na wachache walikubali kupokea hongo kwa 14% (ambao ni 27 kati ya 200)

Katika kitabu hicho, Sikika inatoa mapendekezo kwa Serikali na asasi za kiraia kuandaa miradi mbalimbali ya kuelimisha umma mbinu muhimu za kuzuia na kupambana na rushwa; ili waweze kutambua na kuripoti mapema vitendo vya rushwa. Vilevile haki za mgonjwa ziwekwe wazi.

Serikali ihakikishe uwajibikaji kuanzia ngazi za juu na kuboresha usimamizi kwa kuelezea wa uwazi matarajio na majukumu ya kazi. Pia ihakikishe uwazi, sheria zinazotekelezeka na kuanzisha sera ya upandishaji madaraja ya haki na yenye kuzingatia uwezo

Aidha, kwa mikakati madhubuti ya kupambana na rushwa, msukumo usielekezwe kwenye kupiga marufuku vitendo vya rushwa na kutoa adhabu kwa wakiukaji tu bali pia kwenye kushughulikia mazingira yanayochochea ukuaji wa rushwa na kutoa motisha kwa utendaji mzuri na uadilifu kazini.

Mwisho